# Learning by Ear – Girls' Rights

**Episode 01**

**Title: Education for Girls - A story of Girls' Rights**

**Author: Njoki C. Muhoho**

**Editors: Andrea Schmidt, Katrin Ogunsade**

**Proofreading: Michael Lawton**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**Characters:**

**SCENE 1: FATUMA'S HOMESTEAD**

NARRATOR - 30S MALE

ELDER JACOB - 60: MALE: FATUMA'S FATHER

FATUMA - 14: FEMALE

**SCENE 2: CIRO'S HOMESTEAD**

CIRO – 15: FEMALE

MAMA CIRO - 50: FEMALE

UNCLE BABU - 60: MALE:

NARRATOR - 30S: MALE

**SCENE 3: SCHOOL COMPOUND**

FATUMA - 14: FEMALE

CIRO – 15: FEMALE

CHEPTOO - 15: FEMALE

TEACHER MONA - 35: FEMALE

NARRATOR - 30s: MALE

**SCENE 4: TEACHER MONA'S OFFICE**

| | | | |
|---|---|---|---|
| TEACHER MONA | - | 35: | FEMALE |
| FATUMA | - | 14: | FEMALE |
| CIRO | – | 15: | FEMALE |
| CHEPTOO | - | 15: | FEMALE |
| NARRATOR | | - | 30S: MALE |

**SCENE 5: FATUMA'S HOMESTEAD**

| | | | |
|---|---|---|---|
| CHEPTOO | - | 15: | FEMALE |
| CIRO | – | 15: | FEMALE |
| FATUMA | - | 14: | FEMALE |
| NARRATOR | | - | 30S: MALE |
| 3-4 ELDERS | - | MIXED GENDER, 40-70S | |

**01. <u>MUSIC: THEME MUSIC</u>**

**02. NARRATOR Intro**

Hujambo na karibu kwa sehemu ya kwanza ya mfululizo wa vipindi vya mchezo huu wa Learning By Ear " Noa Bongo Jenga maisha yako kuhusu **"Haki za Wasichana"**. Katika mfululizo wa vipindi kumi kwenye mchezo huu, tunafuatilia maisha ya wasichana watatu ambao ni marafiki wakubwa -Ciro, Fatuma na Cheptoo, wanapokabiliana na changamoto za ujana maishani.Hapana shaka hadithi hii itatufunza mengi kuhusu haki za mtoto wa kike na kutupa hamasa juu ya suala hili.Ama kwa hakika, dunia imewafunza mengi wasichana hawa hususan haki zao za kimsingi na jinsi ya kutatua matatizo yao, wenyewe. Hivyo basi ungana nao katika safari ya kufahamu vyema haki za mtoto wa kike katika makala hii ya kwa kwanza kabisa **"Haki ya kupata Elimu".**

**<u>SCENE 1: FATUMA'S HOMESTEAD</u>**

**03. <u>SOUNDS: UPCOUNTRY FARM SOUNDS</u>**

**04. <u>SFX: DOOR SLAMS. QUICK FOOTSTEPS RUSHING AWAY.</u>**

05. **FATUMA** Kwaheri Mama.. tuonane join!.

**06. <u>SFX: HEAVY BREATHING AND STEPS. BUMP OF COLLIDING BODIES (studio)</u>**

07. **JACOB** Taratibu Mtoto wee! Haraka za nini? Heee...Nenda pole pole!

08. **FATUMA** Samahani Baba..nimechelewa kwenda..

09. **JACOB** Pole pole... !Wewe ni msichana mkubwa sasa, sio mtoto tena! Unafikiri ni mwanamume gani atakubali kumuoa msichana mwenye tabia kama.. ya…ya ...ya..uhunil

10. **FATUMA** Kuolewa?, Baba...! Bado mimi ni mdogo!.. miaka 13 tu..

11. **JACOB** Miaka 13 tu!. Wewe ni msichana mkubwa sasa..haya. tuyaache hayo,..! haraka hizo ni za kwenda wapi?.

12. **FATUMA** **(RUSHING)** Shule zimefunguliwa, na ni mwanzo wa mhula Baba. Na nataka kuwahi shule mapema…tuonane jioni…..!

**13. <u>SFX: FEET RUSHING OFF</u>**

14. **JACOB** (SNEERING and MUTTERING). Shule ...? haah! Shule..? huko ni kupoteza wakati….

15. **NARRATOR.** Ni jambo gani linalo msumbua Mzee Jacob? Yaonekana hafurahii kumuona Binti yake Fatuma akienda shule. Fatuma amekuwa akihisi na tabia hiyo ya Babake kwa muda mrefu lakini anampuuza tu.Hata hivyo lakini, leo tabia hiyo imemkwaza na anajiuliza kwanini Babake hataki aende shule.

Wakati huo huo, katika familia jirani,rafiki yake mkubwa Ciro ana mazungumzo na na Mamake na Mjombake Babu, wanapoendelea kuapta kiamsha kinywa.

**SCENE 2 CIRO'S HOMESTEAD**

16. **SFX: CLATTERING OF CROCKERY AS THEY TAKE BREAKFAST**

| | | |
|---|---|---|
| 17. | **CIRO** | (EXCITED) Mama, Kwa hakika umenifurahisha sana.Huu ni muhula wangu wa mwisho shuleni na hivi karibuni nitajiunga na chuo. |
| 18. | **MAMA CIRO** | Hebu kula kwanza usije ukachelewa! |
| 19. | **UNCLE BABU** | Mmmmm..ni chuo gani hicho unachokizungumzia? |
| 20. | **CIRO** | Lakini Ba-mdogo Babu, nafanya bidii katika masomo yangu ili niweze kujiunga na chuo. Na kisha ni… |
| 21. | **UNCLE BABU** | Tayari nimetoa rubuni. |
| 22. | **CIRO** | (EXCITED) Oh... asante sana Mama!. Hilo ni jambo zuri… katika chuo gani? |
| 23. | **UNCLE BABU** | Ekari mbili za shamba. |
| 24. | **CIRO** | Nini ?Chuo katika ekari mbili za shamba |
| 25. | **MAMA CIRO** | Hapama, anachomaanisha Babako mdogo ni kwamba, tayari ametoa rubuni ya kununua shamba, na wala sio kukulipia karo. |

| | | |
|---|---|---|
| 26. | **CIRO** | (ANGRY) Kwanini lakini? Kwa hiyo sitaweza kuendelea na masomo yangu ya chuo, sivyo? |
| 27. | **UNCLE BABU** | Hapa tuna shamba kubwa sana, na tunahitaji usaidizi zaidi. |
| 28. | **CIRO** | (FRUSTRATED) Mama tafadhali mweleza Ba-mdogo.Nataka kujiunga na chuo kuendeleza masomo yangu.. |
| 29. | **MAMA CIRO** | Wewe Mtoto..! Kuwa na adamu na uwasikize wazazi wako!. |
| 30. | **UNCLE BABU** | Siku moja utaolewa na kuanza familia kwengineko. Kukuelimisha ni kama kupoteza pesa tu!. Tumeamua kununua shamba na wewe utafanya kazi katika shamba hilo… hakuna…hakuna kubisha! |
| 31. | **NARRATOR** | Sasa matatizo yameanza kumuandama Ciro. Huenda akakosa nafasi ya kuendelea na masomo yake. Je atakata tamaa? Hebu tusikie jinsi atakavyoshauriana na wenzake kuhusu changamoto hizi. |

## SCENE 3 SCHOOL COMPOUND

**32. SFX: SCHOOL BELL RINGS. NOISE OF STUDENTS LEAVING CLASSES**

| | | |
|---|---|---|
| 33. | **FATUMA** | (EXCITED) Ciro, Ciro, njoo hapa. |
| 34. | **CIRO** | (EXCITED) Fatuma, …habari swahiba!. Leo mumetoka mapema darasini kuliko sisi!. Sasa.. Ehhh.. na umekuwa mkubwa…! Umeongeza kimo ukiwa likizoni? Umekuwa mrefu….mrefu sana…! |
| 35. | **FATUMA** | Usianze Ciro...! Asubuhi Babangu aliniambia "Hee sasa umekuwa Msichana mkubwa si mtoto tena." |
| 36. | **CIRO** | Ba-mdogo anamipango ya kununua shamba na wala sio kulipia karo. (INTERRUPTION)<br><br>Hee... msikie huyu? |

**37. SFX: STEPS APPROACH**

| | | |
|---|---|---|
| 38. | **CHEPTOO** | Yaani mnazungumzia mashamba na elimu. Kwanini musiishi kama mimi! |
| 39. | **FATUMA/CIRO** | Cheptoo! Umerudi ! |

| | | |
|---|---|---|
| 40. | **CIRO** | Cheptoo,..wewe ni Mtu wa kupenda sifa sana… (IMPRESSED). Kwa sababu shangazi yako anaishi mjini na kumtembelea mara kwa mara wakati wa likizo na mwishoni mwa wiki. Lakini usitusahau sisi rafiki zako wa kijijini. |
| 41. | **CHEPTOO** | Sawa,nimerudi kijijini sasa, sivyo? |
| 42. | **CIRO** | (IMPRESSED)..oooh… oooh…tosha tosha…hebu tazama .., mtindo wake wa nywele, mavazi.. kweli umependeza!. |
| 43. | **CHEPTOO** | Huu ndio mtindo siku hizi…, napendeza sivyo? |
| 44. | **FATUMA** | Cheptoo... huo mtindo wako wa nyele lazima umekugharimu sana.Tazama mavazi yake. Umevalia sketi mpya..na Shati…waonekana unaenda na wakati kabisa hapa shuleni... unakwenda na wakati.Lakini tahadhari mavazi haya hayaruhusiwi hapa shuleni…, yatakukuta? |
| 45. | **CIRO** | Kweli umependeza, lakini nashangaa ni vipi ulivyoweza kuingia darasani asubuhi bila kuonekana na walimu. |

| | | |
|---|---|---|
| 46. | **CHEPTOO** | Mimi sijali? Nywele ni zangu, mavazi… ni pesa za wazazi wangu.. na ni haki yangu!. |
| 47. | **CIRO** | Lakini hapa shuleni kuna sheria zake! |
| 48. | **FATUMA** | Shhhh. (LOUD WHISPER).Jifiche hapa, Mwalimu Mona anakuja!. |
| 49. | **CIRO** | Cheptoo... jifiche hapa...haraka utajikuta mashakani. Mwalimu Mona huyo! |
| 50. | **TEACHER MONA** | Amechelewa,..nimemuona na tayari yumo mashakani. Cheptoo unafahamu vyema sheria za hapa shuleni. Mitindo hiyo ya nywele hairuhusiwi hapa. |
| 51. | **CHEPTOO** | Lakini Mwalimu Mona, huu ndio mtindo wangu ninaopenda...ni … |
| 52. | **CIRO** | (URGENT WHISPER) Cheptoo… shhss nyamaza!. |
| 53. | **TEACHER MONA** | Nataka kumuona nyote ofisini kwangu sasa hivi! |
| 54. | **FATUMA** | Hebu sasa angalia ulivyofanya,Cheptoo. |

55. **NARRATOR** Gumzo la kawaida limewatia mashakani wasichana hawa watatu. Je Cheptoo atasisitiza kuhusu haki zake? Na Je ana haki ya kufanya hivyo? Na ni upi muingiliano wa haki hizi na sheria za shule? Mwalimu Mona bila shaka ana jambo la kuwaeleza. Hebu tuungane nao ofisini mwa Mwalimu Mona.

**<u>SCENE 4 TEACHER MONA'S OFFICE</u>**

<u>64. **SFX: Office sounds, people talking in the background…**</u>

56. **TEACHER MONA** Cheptoo, sujiu nikuadhibu au nikushauri. Nafurahishwa sana na kiwango chako cha ufahamu kuhusu haki zako. Lakini umekosa..! na lazima uadhibiwe.

57. **CIRO** Mwalimu Mona,sasa unatuchanganya. Mara unasema Cheptoo ana haki na kisha bado unataka kumuadhibu.

58. **CHEPTOO** Nadhani ni haki yangu kufahamishwa, kwanini nina haki na upande mwengine sina haki.

| | | |
|---|---|---|
| 59. | **TEACHER MONA** | (STERNLY) Ukiwa mnyenyekevu zaidi, unaweza kujifunza mengi zaidi.Heshima kidogo tu msichana! |
| 60. | **CHEPTOO** | (APOLOGETIC)Samahani, Mwalimu Mona. |
| 61. | **TEACHER MONA** | Nisikilize kwa makini.Kama wasichana wadogo, mna haki zenu za kimsingi. Mfano haki ya elimu, haki ya kujiamulia, haki ya kuchagua na kadhalika. Lakini zaidi mfahamu bado mnaishi miongoni mwa jamii inayoongozwa na sheria zake.Sheria hutungwa kutupa muongozo na utangamano miongoni mwa jamii.Na haki zako pia hazipasi kuwa kiwazo kwa wengine. Ukiendelea kuvaa mavazi haya na mitindo ya ghali ya nywele, bila shaka wenzako watajiona wanyonge na hivyo kuathiri masomo yao. |
| 62. | **FATUMA** | Mwalimu Mona, Cheptoo ni rafiki yangu mkubwa, lakini hunifanya nijihisi maskini sana. Tazama mavazi yangu yalivyochakara na kuraruka. Huwezi kulinganisha na yake?.. yake ni… |

63. **TEACHER MONA** Nasema hivi. Cheptoo, kila mmoja ana haki kuwa hapa shuleni na kupata elimu, Kwa hivyo ni lazime uzingatie sheria za shule…bila ya walakini? Na nikikukuta tena umevalia hivi,sitakubembeleza!. Na nyinyi wengine ni wajibu wenukuzingatia kikamilifu sheria za shule. sawa?

**64. SFX: SCHOOL BELL RINGS**

65. **TEACHER MONA** Sasa.. tokeni hapa ... rudini darasani.

66. **NARRATOR** Je Ciro na Fatuma watakubali masomo yao yatatizwe? Endelea kuwa nasi ufahamu jinsi wanavyo jaribu kutatua matatizo yao

**67. BRIDGE MUSIC**

68. **NARRATOR** Wiki zimepita,Fatuma bado hajafika shuleni. Rafiki zake Ciro na Cheptoo wamenza kuwa na wasi wasi.

69. **CHEPTOO** (WORRIED) Huenda ni nini kilichompata Fatuma? Labda hajisikii vizuri?

70. **CIRO** Sijui. Sina habari. Kama angekuwa hajisikii vizuri, angetuma ujumbe.Si kawaida yake.

71. **CHEPTOO** Habu twende ynumbani kwao baada ya masomol.

72. **CIRO** Sawa twende.

73. **NARRATOR** Baadaye wawili hao wanafunga safari guu moja, mbili hadi nyumbani kwa kina Fatuma. Hawana habari kuhusu yale watakayo kumbana nayo huko. Hata hivyo lakini ni wajibu wao kufahamu matatizo yanayomkuta rafiki yao. Edelea kusikiliza ufahamu yatakayojiri katika safari yao.

**<u>SCENE 5: FATUMA'S HOMESTEAD</u>**

**74. SFX: Sound outside atmosphere, birds, children playing in the background**

75. **CHEPTOO** Ciro, mbona kuna watu wengi nyumbani kwa kina Fatuma.

76. **CIRO** ooh ... Mungu atuepushie..Naomba lisiwe ni jambo baya.Tusongee pale karibu.

**77. <u>SOUND: MUMBLING OF ELDERS</u>.**

78. **CHEPTOO** (WHISPERING) Twende tukachhungulie kwenye dirisha la chumbani mwake.

79. **CIRO** Tazama, wengi wa wageni ni Wazee…Wake kwa Waume..! na wako katika mazungumzo mazito. Unadhani wanajadiliana nini…?

80. **CHEPTOO** Twende tumtafute Fatuma.

**81. <u>SFX: WINDOW OPENING. CLOTHES RUSTLING</u>.**

82. **CHEPTOO** (WHISPERING) sssssppppph…. Ssspppphh Fatuma, uko ndani?.

83. **CIRO** Si uchungulie tu kama yuko ndani?

84. **CHEPTOO** Siwezi kuona vizuri, kuna kiza?

85. **CIRO** Ama labda amefariki na Watu wanapanga maziko yake.

86. **CHEPTOO** Usiseme hivyo… oooh yule pale...! Fatuma… Fatuma… Nini kinachoendelea hapa?

87. **FATUMA** (SCARED VOICE) Cheptoo, Ciro, ni nyinyi? Tafadhali nisaidieni kutoroka hapa.

88. **CHEPTOO** Njoo... Njoo hapa karibu na dirishani, tutakusaidia.

**89. <u>SFX: HEAVING HEAVILY (studio)</u>**

90. **CIRO** (BREATHING HEAVILY) Wewe ni mzito

91. **CHEPTOO** Nilikwambia umekuwa mkubwa.Hebu hema ndani tumbo lako.

92. SFX: MORE HEAVING.

93. **CHEPTOO** Umehema ndani?

94. **FATUMA** (OUT OF BREATH) mmmmmhh

95. **CIRO** Sawa hebu shika hapa... moja , mbili twende…!

96. **FATUMA** (SIGHS OF RELIEF) ooh asanteni sana. Mumemuona?

97. **CHEPTOO** Nani?

98. **FATUMA** Mume wangu mtarajiwa. Ni mmoja wa wale wazee wanaoshauriana pale.Ndio sababu wamenifungia hapa chumbani. Sasa wanashauriana kuhusu mahari ili niolewe na yule Mzee.

99. **CIRO/CHEPTOO** Eti nini?

100. **FATUMA** Ooh hapana, twendeni.. wanakuja, toroka, tukimbie......tukimbie

**101. SFX: QUICK FOOTSTEPS AND PANTING**

| | | |
|---|---|---|
| 102. | **CIRO** | (PANTING)... Cheptoo... sasa tunampeleka wapi wapi? |
| 103. | **CHEPTOO** | (PANTING) Tumpeleke kwa Mwalimu Mona.Atatushauri cha kufanya. |
| 104. | **CIRO** | Ooh nina wasi wasi, kwanza Mamangu na Ba-mdogo wanasema siwezi kujiunga na chuo. Na sasa Fatuma amekatiziwa masomo yake na kuozeshwa Mzee. |
| 105. | **CHEPTOO** | Tunapasa kusimama wima na kutetea haki zetu.Tunapasa kupaza auti zetu kukemea jambo hili. Lakini tutawezeja kufanya hivyo. |
| 106. | **CIRO** | Na hakika Mwalimu Mona atatushauri vyema. |
| 107. | **SFX: NO LONGER RUNNING, URGENT DISCUSSION** | |
| 108. | **FATUMA** | Fanyeni upesi . Siwezi kuolewa mimi. Nataka kuendelea na masomo yangu. |
| 109. | **CIRO** | (PANTING). Hi si sawa.Lazima Mtu ajitokeze kutetea haki zetu. |

| | | |
|---|---|---|
| 110. | **CHEPTOO** | Hapana, sisi wenyewe tunapasa kufanya hivyo.Ni lazima tuzungumze na wenzetu kuhusu haki zetu. Lazima tufahamu haki zetu na kukemea uovu huu. |
| 111. | **FATUMA** | (SADLY) Tafadhali, Cheptoo, Ciro… tuondokeni hapa. |
| 112. | **CHEPTOO** | Sawa twendeni kwa Mwalimu Mona |
| 113. | **CIRO/FATUMA** | Kwa Mwalimu Mona |
| 114. | **RUNNING AGAIN** | |
| **115.** | **THEME MUSIC** | |

## OUTRO

116. **NARRATOR**

Wasichana hao wawili wamefanikiwa kumtorosha rafiki yao nyumbani kwao. Je wamefanya makosa au wanatekeleza haki yao.Lakini ni haki gani wanayopigania? Je Mwalimu Mona atakubali kuwasaidia? Je watafanikiwa kumuokoa Fatuma? na Wazazi wa Fatuma watachukua hatua gani watakapofahamu kwamba  Binti yao ametoroka.

Ili kufahamu mengi zaidi, ungana nasi kwa makala nyingine ijayo kwenye mfululizo wa hadithi hii "HAKI ZA WASICHANA".

Iwapo ungependa kutuma maoni au kusikiliza tena kipindi hiki tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de/lbe.Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa.